SHERIA



Wananchi wakiangalia ajali ya gari iliyotokea kwenye Mlima Iwambi mjini Mbeya. Picha na Maktaba

# Dereva ajali iliyoua 26 Iwambi jela, kulipa faini

Daniel Mjema, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co,tz

**Mbeya.** Mahakama Kuu, Masjala Ndogo ya Mbeya imebariki kifungo cha miaka mitatu jela na faini ya Sh3.7 milioni, alichohukumiwa dereva wa lori, Philipo Mwashibanda aliyesababisha vifo vya abiria 26.

Hukumu hiyo ilitolewa Septemba 22 mwaka huu na Jaji Joachim Tiganga na kuwekwa katika tovuti ya Mahakama jana huku jaji akiitupa rufaa ya dereva huyo na kusisitiza adhabu aliyopewa inastahili.

Juni 7, 2025, eneo la Mlima Iwambi, Barabara Kuu ya Mbeya-Tunduma, dereva huyo akiendesha lori aina ya Scania lenye tela alishindwa kulimudu gari hilo kutokana na uendeshaji wa hatari.

Lori hilo lilikwenda kugongana na basi dogo aina ya Mitsubishi Rosa lililokuwa likiendeshwa na dereva Baraka Samiel Mgalla na kusababisha vifo vya watu 26 waliokuwa katika basi hilo na majeruhi 10.

Alifikishwa mahakamani mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Paul Rupia wa Mahakama ya Wilaya ya Mbeya na kushtakiwa kwa makosa 37 ya uendeshaji wa hatari wa gari na kusababisha ajali iliyoua na kuacha majeruhi.

Kosa la kwanza hadi la 26 lilihusu uendeshaji wa hatari wa lori hilo na kusababisha vifo vya abiria 26 waliokuwa katika basi dogo, kosa la 27 hadi la 36 la kusababisha majeruhi na kosa la 37 la uendeshaji mbaya wa lori uliosababisha ajali hiyo.

Juni 24,2025 alitiwa hatiani baada ya kukiri makosa hayo, kwa kosa la kwanza alihukumiwa kifungo cha miaka mitatu jela na kulipa faini ya Sh100,000 kwa kila kosa kuanzia kosa la kwanza hadi la 36 katika shauri hilo.

Adhabu hiyo iliamriwa kutumikiwa kwa pamoja alitakiwa kutumikia kifungo cha miaka 108 na kulipa faini ya Sh3.6 milioni, lakini kwa kuwa vifungo viliamriwa kutumikiwa pamoja, atatumikia miaka mitatu jela na kulipa faini ya Sh3.6 milioni.

Katika kosa la 37, alihukumiwa kifungo cha miaka mitatu na kulipa faini ya Sh100,000.

**Alivyopambana kujinasua**

Baada ya kuhukumiwa, kupitia kwa Wakili Philip Mwakilima, Mwashibanda hakuridhishwa na hukumu hiyo akaamua kukata rufaa akiegemea sababu kuu nne za rufaa kupinga kutiwa kwake hatiani na adhabu aliyopewa.

Alijenga hoja kuwa hakimu aliyemhukumu alikosea kisheria na kimantiki pale aliposhindwa kuzingatia taratibu sahihi wakati wa kumtia hatiani na kumhukumu.

Pia, kupitia kwa wakili huyo, dereva huyo alieleza kuwa hakimu alikosea kisheria na kimantiki kwa kushindwa kumpa nafasi mrufani kubishania maelezo yaliyosomwa na upande wa jamhuri au kupewa nafasi ya kuongeza katika maelezo hayo.

Halikadhalika alilalamika kuwa, hakimu alikosea kisheria na kimantiki pale aliposhindwa kuzingatia kuwa, wakati wa maombolezo (mitigation), mtuhumiwa aliibua utetezi fulani na hakimu alitakiwa abadili kukiri kwake kosa.

Mwisho, alidai hakimu alikosea kisheria na kimantiki kwa kushindwa kufafanua visababishi vya makosa ambayo mrufani alikuwa akishtakiwa nayo, lakini pia alishindwa kurekodi kile ambacho mrufani alikieleza kuhusu makosa hayo.

Upande wa jamhuri ukiwakilishwa na Wakili wa Serikali, Salmin Zuberi ulipinga sababu hizo za rufaa, akishikilia msimamo kuwa hakuna rufaa inayoweza kukatwa kutokana na mshtakiwa mwenyewe kukiri makosa yake.

Wakili huyo alisema mashtaka dhidi ya mrufani yalisomwa kwa Kiswahili anachokielewa vizuri na akajibu ni kweli alisababisha ajali na vifo na baadaye alikiri shtaka moja baada ya lingine kadri alivyosomewa na upande wa mashtaka.

**Hukumu ya jaji ilivyokuwa**

Katika hukumu yake, Jaji Tiganga alisema baada ya kupitia kwa umakini kumbukumbu za usikilizwaji wa shauri hilo, sababu za rufaa na mawasilisho ya pande mbili, hoja ya kutolewa uamuzi inahusiana na mrufani kukiri kosa.

Jaji alisema hoja ni kama kukiri kwake huko kulichukuliwa kwa usahihi na hakimu aliyesikiliza shauri hilo na kama ilitosheleza kumtia hatiani mrufani.

Alieleza kuwa, katika shauri hilo, mwenendo wa kesi hiyo unaonesha hati ya mashtaka ilisomwa kwa mrufani na kuelezewa kwa Kiswahili na mrufani akajibu (akinukuu alichojibu mahakamani) "Kweli na sahihi, nimesababisha ajali na vifo."

"Baada ya kusomewa shitaka, upande wa jamhuri ulielezea maelezo ya kosa kuwa aliendesha lori aina ya Scania na kugongana na Mitsubishi Rosa na kusababisha vifo 26, majeruhi 10 na kuharibu magari na akakubali maelezo hayo," alisema jaji.

"Kwa mtazamo wa Mahakama hii, utaratibu ulizingatia kikamilifu kifungu cha 245(2) cha CPA (Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai) na kukiri kwake kulirekodiwa kwa usahihi na hakuweza kukosolewa," alieleza Jaji Tiganga.

"Kwa kuongezea, makosa yote yalisomwa moja baada ya lingine, ikifuatiwa na maelezo ya kina ya kila kosa kwa lugha ya Kiswahili ambayo mrufani kila alipoulizwa aliyathibitisha maelezo hayo kuwa ni sahihi," alisisitiza jaji.

Zaidi ya hayo, alisema uzito wa ushahidi wa jamhuri uliongezewa na kuwasilishwa kwa vielelezo zikiwamo taarifa za uchunguzi wa vifo (postmortem reports), maelezo ya onyo ya mshtakiwa, PF 3 na ramani ya eneo la ajali.

"Kila kielelezo kilisomwa mahakamani na kilivyowekwa mbele yake (mrufani) alijibu na kukiri kuwa ni kweli maudhui ya nyaraka hizo ni sahihi,"alisema jaji Tiganga katika hukumu yake hiyo akibariki hukumu ya Mahakama ya Wilaya.

Ni kwa msingi huo, jaji alisema ameridhika kuwa, kulikuwa hakuna dosari za kisheria na kwamba, kutiwa hatiani kwa mrufani huyo kulikuwa ni sahihi kisheria na adhabu aliyopewa ilikuwa sahihi kisheria.

> "Kila kielelezo kilisomwa mahakamani na kilivyowekwa mbele yake (mrufani) alijibu na kukiri kuwa ni kweli maudhui ya nyaraka hizo ni sahihi."
>
> Jaji Joachim Tiganga

**FAHAMU**

Mahakama Kuu ya Tanzania, Masjala Ndogo ya Mbeya imethibitisha hukumu ya kifungo cha miaka mitatu jela na faini ya Sh3.7 milioni dhidi ya dereva wa lori, Philipo Mwashibanda, aliyesababisha ajali Juni 7, 2025 katika eneo la Mlima Iwambi, Mbeya.

Ajali hiyo ilisababisha vifo vya watu 26 na majeruhi 10 baada ya lori alilokuwa akiendesha kugongana na basi dogo la abiria.

Mwashibanda alikiri makosa 37, ikiwamo uendeshaji hatarishi, mbele ya Mahakama ya Wilaya ya Mbeya na kuhukumiwa kifungo cha miaka mitatu jela kwa kila kosa, lakini vifungo hivyo viliamriwa kutumikia kwa pamoja.

Alikata rufaa akidai hukumu haikuzingatia taratibu za sheria, lakini Mahakama Kuu kupitia Jaji Joachim Tiganga ilikataa hoja hizo na kusisitiza kuwa haki ilizingatiwa, ikiwamo maelezo ya kukiri na vielelezo vya ushahidi.

CamScanner

Nipashe, Ijumaa Septemba, 26, 2025 pg 6

## Muungwana Lazima Nilonge

# Hili la kupunguza ajali, madereva wajibikeni, wapitia njia tusijisahau

**KWA** hili lazima tuambiane kweli. Kumekuwapo tabia endelevu, nikiwaona wote kuanzia madereva wa magari, pikipiki, bajaji hata baiskeli katika barabara zetu mijini, sasa inakuwa kero ya namna yake.

Hali ya kutozingatia njia zenu, ni hatari kwa maisha ya wengine, kwani ni chanzo cha wazi kwa ajali.

Kwa ukweli kabisa, ndugu zangu mnatakiwa kuzingatia kanuni za usalama. Kila mmoja anatakiwa kutambua eneo lake la kupita na sio kusubirli kuambiwa.

Ni tabia inayoanzia kwa madereva wote nchini. Namkumbuka Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akaagiza Wizara ya Ujenzi kufanya maboresho katika ujenzi wa miundombinu ya barabara nchini.

Kimsingi, ni suala la kuhakikisha wanaongeza njia za waendao kwa miguu, pia wanaoendesha pikipiki na baiskeli ili kupunguza ajali za barabarani.

Ni agizo lake la Agosti 26, mwaka jana jijini Dodoma, katika ufunguzi wa Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani nchini, inayoenda sambamba na Maadhimisho ya Miaka 50 ya Baraza la Taifa la Usalama Barabarani.

Dk. Mpango akasisitiza kutocheleweshwa uwekaji mawe ya mipaka ya barabara, katika hifadhi za barabara kwa miradi inayojengwa, ili kuilinda na kuzuia uvamizi wa barabara hizo.

"Muangalie usanifu wenu na kuhakikisha barabara zote zinakuwa na njia za watembea kwa miguu hasa mijini.

"Pia, njia za waendesha baiskeli na pikipiki", hakikisheni hili mnalisimamia", akaelekeza Makamu wa Rais.

Makamu wa Rais Dk. Mpango, akataka Baraza la Taifa la Usalama Barabarani kushirikiana na Polisi, kuhakikisha wanasimamia ukaguzi makini wa vyombo vya moto mwaka mzima na sio kusubiri kipindi cha Wiki ya Nenda kwa Usalama.

**Hapo napo tukasikia sauti wadau waandamizi wa Baraza La Taifa la Usalama Barabarani, kwamba jitihada za kupambana na makosa ya kibinadamu yanayochangia ajali, leo hii inasherehekewa miaka 50.**

Aidha, akaeleza ili kupunguza ajali za barabarani zinazosababishwa na Makosa ya Kibinadamu, ni vyema madereva kuongeza umakini na kudhibiti vihatarishi vya ajali barabarani.

Kuzingatia nui msomo aliyezama katika elimu ya Uchumi, akaamua kuzama katika kielelezo cha takwimu, akionyesha mwaka 2023 ajali zilikuwa 1,733 na zikaua watu 1,647 na majeruhi wakawa 2.716.

Hapo ndipo Waziri wa Mambo ya Ndani ya nchini, Hamadi Masauni, anaungana naye, akisema uwapo wa matumizi ya mifumo ya teknolojia ya habari na mawasilano, inapunguza ukiukwaji maadili kwa madereva, pia watembeao kwa miguu.

Hapo napo tukasikia sauti wadau waandamizi wa Baraza La Taifa la Usalama Barabarani, kwamba jitihada za kupambana na makosa ya kibinadamu yanayochangia ajali, leo hii inasherehekewa miaka 50.

Mkurugenzi wa Usalama na Mazingira kutoka Wizara ya Ujenzi, Mhandisi Kashinde Musa, anasema katika bajeti ya taifa ya mwaka 2024/2025, Wizara ya Ujenzi ikatenga bajeti ya kupunguza msongamano katika majiji matano na kusisitiza ni usanifu utakaofanywa kuzingatia watembea kwa miguu, waendesha baiskeli na pikipiki.

Ni vyema kuzingatia maelekezo ya waenda kwa miguu mnatakiwa kupita njia rasmi ili kuepukana na hili janga ambalo ni msumeno, unaoakata huku na kule.

Hivyo, tuangalie rusije tukapata madhara yanayoepukika, badala ya kukatribisha kuanzia vifo, ulemavu wa kudumu na lindi la hasara.

Madereva msijisahau barabarani. Sote tuna haki ya kutumia barabara, kuanzia waendao kwa miguu nao wana haki, pia sababu za uhuru huo kutumia barabara.

Ombi langu kwa waziri yeyote atakayebeba dhamana hiyo, awasaidie waendao kwa miguu watumie vyema njia kisheria, ili kuepusha magari na pikipiki zisipite mahali waliko waendao kwa miguu, hali inayoepusha ajali tunazoweza kuzikwepa.

Nipashe, Ijumaa, Septemba, 26, 2025 pg 6

CamScanner